TANGAZO LA SERIKALI NA.182 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MPUNZE YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Mpunze ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mipango ya jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 336 yenye majira – nukta 430656MS, 9564091KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KS60°27'17"MS kwa umbali wa kilomita 9.39 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV367 yenye majira - nukta 438828MS, 9568724KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS41°23'46"MG kwa

*Tangazo la Serikali Na. 182 (Linaendelea)*

umbali wa kilomita 6.43 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 331 yenye majira - nukta 434524MS, 9573651KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KS51°44’31”MG kwa umbali wa kilomita 6.88 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 334 yenye majira - nukta 429167MS, 9569288KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS15°59’26”MS kwa umbali wa kilomita 5.4 hadi ulipoanzia.”

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*